# *BARUA #06;JINSI YA KUFIKA NGAZI ZA JUU ZA UFANISI.*

Karibu rafiki yangu ninayekupenda sana kwenye barua yetu ya mafanikio.

Kwenye barua ya leo, nakwenda kukushirikisha jinsi ya kufika ngazi za juu za ufanisi ili uweze kufikia ndoto kubwa uliyonayo.

Kila mmoja wetu ana ndoto kubwa anayofanyia kazi kwenye muongo huu tuliopo sasa wa 2020 – 2030. Ndoto hizi ni kubwa kiasi kwamba ukiwaambia wengine wanaona kama umechanganyikiwa.

Wewe mwenyewe ukiitafakari ndoto yako kubwa, unaona kama unajidanganya, unajiuliza kama kweli utaweza kuifikia, kwa sababu hakuna aliyekuzunguka ambaye amewahi kufika ndoto za juu kama hizo.

Hivyo imani yako pekee ni kikwazo kwako kufika ndoto kubwa uliyonayo na wale wanaokuzunguka ndiyo kikwazo kikubwa zaidi.

Lazima uwe na njia ya kuvuka vikwazo hivi, uweze kufika ngazi za juu za kufikiri na kuchukua hatua ili uweze kufikia ndoto uliyonayo.

## Unachotaka.

Kile ambacho kila mmoja wetu anataka ni kufikia ndoto kubwa aliyonayo, kutimiza kusudi la yeye kuwa hapa duniani.

Hata wale wanaoonekana kutokufanya chochote, bado wana hitaji hilo, ila wanachokwama ni njia ya kuweza kufika wanakotaka kufika.

## Vikwazo vitatu.

Kuna vikwazo vikubwa vitatu vinavyokuzuia wewe kufika kule unakotaka kufika.

Kikwazo cha kwanza ni hali ya kutokuwa na uhakika. Hakuna jambo lolote duniani lenye

uhakika, hivyo kama kuna wakati unajiona kama huwezi kufika unakotaka kufika, uko sahihi kabisa. Hata kwenye sayansi, hakuna jambo lolote lenye uhakika. Lakini bado watu wanafanya makubwa. Kwa kutokujua kutokuwa na uhakika ni hali ya kawaida, wengi wamekuwa wanakata tamaa na kuishia njiani.

Kikwazo cha pili ni ukinzani. Kuna ukinzani wa aina mbili, wa ndani na wa nje. Ukinzani wa ndani unaanzia kwako mwenyewe, kwa kujiwekea vikwazo ili usichukue hatua. Inaweza kutokana na ugumu unaouona kwenye safari, inaweza kuwa hofu ya kushindwa au hofu ya kufanikiwa. Ukinzani wa nje unatoka kwa wale ambao hawajawahi kufanya makubwa, na hivyo hawaamini wengine wanaweza kufanya makubwa. Bila ya kujua aina hizi za ukinzani, utajikuta hupigi hatua na unabaki hapo ulipo wakati wote.

Kikwazo cha tatu ni kuahirisha. Binadamu huwa tuna tabia ya kuahirisha mambo, hasa pale jambo linapokuwa halina uhakika na lina ugumu kufanya. Huwa tunaona hatujawa tayari,

au siku zijazo ndiyo sahihi zaidi. Lakini kinachotokea ni ukishaahirisha kitu inakuwa tabia, ni vigumu mno kuja kukifanya. Bila ya kujua kuahirisha ni kikwazo, hutaweza kupiga hatua kubwa.

Vikwazo hivi vitatu vinamkabili kila mtu, waliofanikiwa na walioshindwa. Lakini waliofanikiwa wamekuwa wanavikabili na kupiga hatua, huku walioshindwa wakikubali kuangushwa navyo.

## Hatua saba za kufikia ufanisi wa juu.

Kwa ndoto kubwa uliyonayo na vikwazo vinavyokukabili, hapa kuna hatua saba za kuchukua ili uweze kufikia ufanisi wa juu, uweze kuchukua hatua ili kufikia ndoto hiyo kubwa.

### Anza na hadithi unayojiambia.

Kila mmoja wetu kuna hadithi ambayo anajiambia, hadithi hiyo ndiyo imani uliyonayo kuhusu maisha na wewe mwenyewe na hadithi hiyo ndiyo inaamua kiwango cha mafanikio utakayofikia.

Kwa walio wengi, hadithi wanazojipa ni za ukomo na hivyo zinakuwa kikwazo kwao kufanikiwa.

Unapojifikiria, unajiona mtu wa aina gani? Je unajiona mtu wa chini, uliyepitia mateso mengi na huna nafasi ya kufanya makubwa?

Je unajiona mtu asiye na elimu kubwa na hivyo huwezi kufanya makubwa?

Au unajiona mtu wa hadhi ya chini, usiyestahili na popote ulipofika sasa ni bahati tu?

Kuna hadithi ambayo umekuwa unajiambia maisha yako yote, huenda jamii ilikufundisha au maisha uliyokulia yamekujenga hivyo.

Huu ni wakati wa kuitafakari hadithi unayojiambia, picha unayoipata kuhusu wewe na kuivunja ili isiwe kikwazo kwako.

Tengeneza hadithi yako mpya, hadithi ya kujiona ukiwa na uwezo na nguvu za kufikia ndoto kubwa uliyonayo. Chochote ambacho umepitia huko nyuma usikubali kiwe kikwazo kwako. Badala yake kuwa huru sasa, jua una

fursa kumbwa mbele yako ya kuwa vile unavyotaka kuwa.

## Kabiliana na unachokikwepa.

Kila mmoja wetu kuna kitu ambacho anakikwepa kwenye maisha yake. Hicho ni kitu unachohofia sana na hutaki kukikabili. Kile unachokikwepa ndiyo kikwazo kikubwa kwako kufikia ndoto zako kubwa. Kwa sababu kinakujengea hofu ambayo haitakuruhusu uwe huru kuchukua hatua unazotaka.

Ni wakati wa kukabiliana na kile unachokikwepa au kukihofia.

Anza kwa kuorodhesha hofu kubwa kabisa ambazo unazo. Ni nini kinakunyima usingizi usiku? Ni kitu gani ukishakifikiria tu unakosa nguvu ya kuendelea?

Ubaya ni kwamba unachokwepa huwa kimejificha na siyo rahisi kujua. Huwa kimejengeka ndani yako kutokana na maisha ambayo umeyaishi tangu ukiwa mtoto na kujengwa na mazingira mbalimbali ambayo umepitia.

Kwa mfano unaweza kuwa unapanga kuanza aina fulani ya biashara lakini hufanyi hivyo. Au hata ukianza hupigi hatua na kufanikiwa. Kumbe ndani yako una hofu kubwa ya biashara, ambayo uliipata baada ya kumwona mtu wa karibu akianguka kibiashara na maisha yake kuwa magumu. Hivyo ukajiambia biashara siyo nzuri.

Kadhalika unaweza kuwa huna mahusiano mazuri na wengine kwa sababu ndani yako una hofu kubwa ya kuumizwa, uliyojijengea baada ya kuumizwa kwenye mahusiano ya nyuma.

Kuna hofu zimejificha ndani yako, ambazo zinakufanya ukwepe baadhi ya vitu ili usizikabili, ni wakati wa kuchimba hofu hizo na kutokuziruhusu ziwe kikwazo kwako.

## Jiamini.

Jaribu kufanya kitu chochote kikubwa na dunia itakujaribu, kitu cha kwanza ambacho dunia inajaribu kwako ni kwa kiasi gani unajiamini. Kama hujiamini wewe mwenyewe, hutaweza kufikia ndoto kubwa uliyonayo.

Kwa sababu kitendo tu cha kuchukua hatua ili kufikia ndoto kubwa, kinakugeuza kuwa adui wa jamii nzima. Kila mtu atakukabili kwa upinzani wa hali ya juu, kukukatisha tamaa na kukuonesha ni jinsi gani huwezi au utashindwa.

Kama hiyo haitoshi, dunia itakutisha kweli kweli, itakuwekea vikwazo vikubwa. Unaweka mipango yako vizuri, unachukua hatua sahihi lakini matokeo yanakuja tofauti kabisa na ulivyotegemea.

Kama hujiamini, utaishia kukubaliana na wale waliokuambia huwezi au haiwezekani na utachagua kurudi kwenye maisha ya kawaida.

Unapaswa kujiamini mno, kwa kiwango ambacho wengine wataona una kiburi au wendawazimu. Pamoja na magumu unayokuwa unapitia, pamoja na kushindwa unakokabiliana nako, usitilie shaka imani yako kwako.

Amini unaweza, amini utaifikia ndoto kubwa na amini chochote unachopitia ni maandalizi ya kukabidhiwa ushindi mkubwa wa ndoto yako.

## Jijengee nidhamu binafsi.

Kwenye hii dunia una machaguo mawili, kufanyia kazi ndoto yako au kufanyia kazi ndoto za wengine. Kama unaweza kujisimamia mwenyewe, kujisukuma na kujiadhibu, utaweza kufanyia kazi ndoto yako. Kama huwezi, basi utalazimika kufanyia kazi ndoto za wengine, ambao watakusimamia, watakusukuma na kukuadhibu.

Kama umeajiriwa au umewahi kuajiriwa unajua kabisa ni jinsi gani mwajiri au bosi wako hataki mchezo. Unajua kabisa kwamba unapaswa kuwahi kazini asubuhi, unapaswa kutekeleza majukumu uliyopangiwa ndani ya muda na wakati mwingine kufanya kazi kwa muda wa ziada pale inapohitajika.

Chini ya uangalizi wa wengine wengi huwezi kufanya hayo, lakini wakiwa wenyewe, kwenye shughuli zao wenyewe, hawawezi kuyafanya hayo, na hilo ndiyo linawazuia kufikia ndoto zao kubwa.

Lazima ujijengee nidhamu binafsi, ujichague wewe kuwa mwajiri wako mwenyewe ambaye hana huruma kabisa. Ujipangie yale unayoyafanya na wakati utakapoyafanya na kisha kujisimamia kuyafanya kama ulivyopanga bila ya kujipa sababu yeyote.

Uweze kujiadhibu mwenyewe pale unapokwenda tofauti na ulivyopanga ili wakati mwingine usirudie hivyo.

Kama hujafika hatua ambayo wengine wakiangalia unavyofanya wanasema unajitesa, hujaweza kujenga nidhamu binafsi ya hali ya juu. Lazima ujifanye kuwa mtumwa wako mwenyewe hasa, maana ukijiendekeza, utaishia kubaki pale ulipo.

## Jijengee maadili na viwango vya juu.

Nidhamu ni vile unavyofanya, maadili na viwango ni vile unavyoendesha mambo yako. Sifa yako ni hitaji muhimu mno kwenye mafanikio yako, na inajengwa kwa viwango ulivyojiwekea na nidhamu uliyonayo.

Hakikisha una maadili na viwango vya juu ambavyo unavisimamia kwenye maisha yako. Yeyote anayejihusisha na wewe anajua kabisa unasimama upande upi, bila ya kuwa na wasiwasi kama umebadilika au la.

Anza na kuwa mwaminifu na mwadilifu, fanya neno lako kuwa sheria, ukisema unatekeleza bila ya kutoa sababu yoyote ile. Ukiwa na sifa hii ya kutekeleza kila unachosema, utaaminika na wengi na kupata fursa nzuri zaidi.

Mara zote fanya na kusimamia kile kilicho sahihi, hata kama kina manufaa kiasi gani, kama siyo sahihi usikifanye. Jina na sifa yako ina thamani kubwa kuliko manufaa ya muda mfupi utakayoyapata kwa kufanya yale yasiyo sahihi.

Jali maslahi ya wengine na hakikisha kila unayejihusisha naye anatoka kwako akiwa amenufaika. Jijengee sifa ya mtu anayewanufaisha wengine na siyo mtu anayejinufaisha kupitia wengine. Kuwanufaisha wengine kunakupa fursa nzuri na kubwa kwa baadaye.

Cheza mchezo wa muda mrefu, chochote unachofanya, angalia matokeo na madhara yake kwa muda mrefu. Kumbuka ndoto yako siyo kitu cha leo na kesho, ni kitu cha miaka 50 na zaidi ijayo. Je uko tayari kufanya kitu kitakachokunufaisha leo na kesho na kikawa kikwazo kwako kwa miaka 10 ijayo?

Mwisho jihusishe na watu ambao wana maadili na viwango vya juu pia. Epuka sana wale ambao hawana maadili, mfano wasio waaminifu, wanaotaka kujinufaisha zaidi na wanaotafuta njia za mkato. Ukiwaendekeza watu hao, hasa wanapokuwa wa karibu, wanaweza kukushawishi ukajikuta unafanya usichotaka. Ukishagundua mtu hana maadili na viwango vya juu kama unavyoishi wewe, kaa naye mbali. Dunia ina watu zaidi ya bilioni 7, usijidanganye hakuna walio na viwango kama vyako, watafute, wapo wengi tu.

## Ishi siku yako moja kwa ukamilifu.

Kulala masikini na kuamka tajiri ni hadithi tu. Mafanikio ya haraka ni kauli ya mauzo inayotumika kuwahadaa watu kununua vitu

fulani. Mafanikio ya kweli yanachukua muda na hatua ndogo ndogo. Jinsi unavyoiishi siku yako moja, ndivyo unavyoyajenga maisha yako.

Pamoja na ndoto kubwa ulizonazo, hazitatokea kwa siku moja, bali zitajengeka kwa hatua unazochukua kila siku.

Hivyo kwa kila siku yako moja, ishi kwa ukamilifu wake.

Kuwa na mambo ambayo unayafanya kila siku katika kuelekea kwenye ndoto yako.

Jijengee utaratibu ambao utauishi kila siku, ambapo unajua lazima utafanya na siyo kuanza kubishana na wewe mwenyewe iwapo unafanya au la.

Kwenye kila siku yako kuna yaliyopita utakayoona hukufanya kwa usahihi na yajayo ambayo utakuwa unayahofia. Lakini usipoteze muda wako kwenye jana wala kesho, ishi kwenye wakati uliopo.

Muda wako ndiyo kitu cha thamani zaidi kwako, ukishaupoteza haurudi tena. Upangilie muda wako vizuri na ulinde.

Kila wakati utakuwa na mambo mengi ya kufanya kuliko muda ulionao, weka vipaumbele vyako vizuri na fanya yale tu yaliyo muhimu kufikia ndoto yako kubwa.

Unachopaswa kuangalia ni siku uliyonayo, jinsi ya kuitumia vizuri ili kuweza kuiishi kwa ukamilifu wake na kujisogeza karibu na ndoto yako. Ukikamilisha siku yako nenda inayofuata kwa mpango huo huo.

Kabla hujaianza siku yako jipe vipaumbele vyako kwenye siku hiyo, orodhesha yale unayokwenda kufanya kwenye siku hiyo na hayo ndiyo unapaswa kuhangaika nayo.

Unapoimaliza siku yako jifanyie tathmini, orodhesha yale yote uliyofanya kwa siku nzima. Kisha tathmini yapi umefanya vizuri na yapi hukufanya vizuri. Angalia yapi utaendelea kufanya na yapi utaachana nayo. Na pia jua

maeneo gani unahitaji kuboresha zaidi kwenye siku zinazofuata.

Unapoitathmini kila siku yako, unaona mapema makosa unayofanya na kuyarekebisha kabla hayajawa na madhara makubwa.

## Kuwa na mtazamo chanya kwa kila kitu.

Mtazamo wako ndiyo kila kitu, mtazamo wako ndiyo utakaoamua kama haya yote uliyojifunza hapa yatafanya kazi au la.

Mtazamo ni kitu unachochagua, lakini kina madhara makubwa kwenye hatua unazokwenda kuchukua na matokeo utakayoyapata.

Kuwa na mtazamo chanya kwenye kila kitu, ndiyo, kila kitu kichukulie kwa namna chanya.

Haijalishi ni kitu ulichotaka au la, haijalishi ni kitu chenye faida au hasara kwako, kila kitu kichukulie kwa mtazamo chanya.

Iko hivi, dunia huwa inafanya mambo yake kwa namna yake, kila kinachofanywa na dunia ni sahihi. Ila sisi kwa matakwa yetu huwa

tunayatafsiri kama mazuri au mabaya, sahihi au siyo sahihi.

Kuanzia sasa, wajibu wako ni kupokea kila kinachotokea kwenye maisha yako kama kinavyokuja, na kuwa na mtazamo chanya juu ya kitu hicho.

Umepata hasara, usiichukulie kama kupoteza, bali chukulia kama funzo, chukulia kama ada uliyolipa kujifunza kitu gani kisichokuwa sahihi kufanya. Na hapo kaa chini kweli ujue nini kimepelekea wewe kupata hasara hiyo na ondoka na somo ni namna gani ya kuepuka kupata hasara kama hiyo.

Mtu uliyemuamini amekuangusha au kukuumiza chukulia kwa namna chanya, shukuru umemjia mapema kabla hujampa nafasi kubwa zaidi ambapo angekuangusha na kukuumiza zaidi.

Chochote kile unachopitia, hata kama wengine wanakiona ni kibaya kiasi gani, wewe kichukulie chanya. Kama bado upo hai, una cha kujifunza na kuweza kuwa bora zaidi wakati ujao.

Unapoangalia kila kitu kwa mtazamo chanya, unajipa jukumu juu ya kitu hicho, unapata nafasi ya kujifunza na kuweza kuwa bora zaidi. Unapoangalia kwa mtazamo hasi, unawalaumu wengine, unakwepa majukumu yako, hujifunzi na hivyo kitu hicho kinaendelea kutokea kwako zaidi na zaidi.

Kwa kila kinachotokea, kwa namna dunia inavyoenda, chukulia chanya, chukulia ni dunia inakupa funzo na kukuimarisha ili uweze kupokea mafanikio yako makubwa.

## Hutaeleweka.

Kama kuishi ndoto yako kubwa kunawafanya wengi wasikuelewe, basi kutekeleza haya saba kutawafanya wasizidi kukuelewa.

Wengi watakuchukulia kama mtu uliyechanganyikiwa, mtu unayejidanganya.

Lakini unachopaswa kujua ni kwamba kila mtu kwenye maisha kuna kitu anajidanganya nacho.

Je ni bora ujidanganye kwa kitu kisicho na manufaa au ujidanganye kwa kitu chenye

manufaa. Mwanzoni utaonekana kujidanganya, lakini kadiri unavyokwenda unajenga tabia ambazo ni imara kweli kweli na tabia hizo zitakuwezesha kufikia ndoto zako kubwa.

Unachopaswa kujua ni kwamba wale ambao hawakuelewi sasa, wanakupinga na kutaka kukuangusha, ndiyo watakaoshangilia siku ukifanikiwa. Ndiyo watakaokuambia kwamba walijua utafanikiwa.

Hivyo hupaswi kuwasikiliza sasa, kama ambavyo pia hupaswi kuwasikiliza utakapofanikiwa.

Wewe unachotaka kufikia ni ndoto zako kubwa, kutimiza kusudi lako, wengine wanasemaje hilo halikuhusu. Hakuna anayejua unataka nini hasa na hakuna anayejua uwezo mkubwa ulio ndani yako.

Wengi wanaokushauri nini unaweza au huwezi kufanya, wao wenyewe hawajui nini wanaweza au hawawezi kufanya. Mbaya zaidi hawajui hata wanataka nini, wanayaendesha maisha yao kwa kufuata mkumbo na wanakasirika sana

wanapoona wewe hufuati mkumbo kama wewe.

Utaanguka na kushindwa, watakuambia walijua hutafika mbali, lakini utasimama na kuendelea tena.

Kila wakati kazana kuwa bora zaidi ya ulivyokuwa jana, usishindane wala kujilinganisha na wengine. Pambana kuwa wewe, ambaye ni bora zaidi kadiri muda unavyokwenda.

Hakuna anayeweza kuwa wewe na wewe huwezi kuwa kama mwingine yeyote, chagua kuyaishi maisha yako, chagua kupambana, chagua kuteseka, kwa sababu unajua nini unataka, na unajua utakipata kwa sababu uko kwenye njia sahihi.

Ukishakuwa kwenye njia sahihi, kinachohitajika ni muda tu, ambao unajipa na huhangaiki kabisa na njia za mkato.

Fanyia kazi haya uliyojifunza hapa, ili uweze kwenda ngazi za juu kabisa kifikra na kimatendo na uweze kufikia ndoto zako kubwa.

## MAONI, SHUHUDA NA MASWALI.

Karibu kwa maoni, shuhuda na maswali kuhusu barua hii.

Kama kuna mahali hujaelewa na ungependa ufafanuzi zaidi basi karibu uulize swali.

Kama kuna eneo unaweza kuongeza maoni zaidi karibu pia.

Na kama una ushuhuda wa namna umewahi kufanyia kazi yale uliyojifunza kwenye barua hii, karibu utushirikishe matokeo ambayo uliyapata.

Maoni, maswali na shuhuda viwekwe moja kwa moja kwenye kundi la KISIMA CHA MAARIFA wasap.

Nikutakie kila la kheri katika kufanyia kazi haya uliyojifunza kwenye barua hii.

Rafiki yako anayekupenda sana,

Kocha Dr. Makirita Amani,

www.amkamtanzania.com/kocha

0755 953 887 / kochamakirita@gmail.com

**MUHIMU;** KAMA HUJAPATA BARUA ZA NYUMA, FUNGUA; www.kisimachamaarifa.co.tz/barua2021